

Makosa ya Kimatamshi Yanayofanywa na Wazungumzaji wa Kiswahili wa Mkoa wa Mara nchini Tanzania

Nyanjura Sabato
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Ikisiri

Makala haya yamechunguza makosa ya kimatamshi yanayofanywa na wazungumzaji wa Kiswahili wanaoishi katika mkoa wa Mara nchini Tanzania. Suala hili linasababishwa na changamoto ambazo wanakumbana nazo wazungumzaji katika harakati za kujifunza Kiswahili ambayo ni lugha yao ya pili (L2). Hata hivyo, katika harakati za kuzungumza Kiswahili wazungumzaji hao wamejikuta wakikabiliwa na makosa ya udondoshaji wa baadhi ya sauti, uchopekaji wa sauti na ubadilishaji wa sauti. Dane (1990) anaeleza kuwa mwingiliano wa lugha unahatarisha lugha kwani husababisha lugha moja kubadilika, kuchanganyika na lugha nyingine hata kufa. Aidha, imebainika kuwa makosa hayo husababishwa na sababu kadhaa ambazo zimewafanya wazungumzaji hao kutumia kimakosa kanuni za lugha ya Kiswahili. Mbinu za mahojiano na dodoso zilitumika kupata data za utafiti huu. Uchunguzi huu umeongozwa na Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia iliyoasisiwa na Chomsky na Morris (1968). Nadharia hii ilitusaidia kubaini makosa ya udondoshaji wa sauti, uchopekaji wa sauti, ubadilishaji wa sauti na sababu za kuwapo kwa makosa hayo. Khansir (2012) anabainisha kuwa kila lugha ina muundo wake wa sauti na mpangilio wa maneno. Uhamishaji wa muundo wa lugha ya kwanza katika lugha ya pili hudhihirika kama makosa. Kutokana na mwingiliano huo wanajamiilugha waliopo katika mkoa wa Mara wamekuwa wakizungumza lugha ya Kiswahili huku wakiwa wanakabiliwa na baadhi ya makosa.

Maneno Muhimu: *Matamshi, Kiswahili, Tanzania, Lugha yao ya Pili, Uchopekaji, Jamiilugha*

Utangulizi

Mkoa wa Mara unapatikana kaskazini mwa Tanzania. Wananchi wanaoishi katika mkoa huu ni wanajamii lugha mbalimbali. Kila jamii ina lugha yake ya kwanza, yaani lugha mama, ambayo inaiongoza jamii hiyo katika mawasiliano na katika kuendesha shughuli za uzalishaji mali. Chimera (1998) anaeleza kwamba lugha mama ni ile ambayo mtu hujifunza kwa mara ya kwanza kabisa maishani mwake kabla ya kujifunza lugha nyingine yoyote ile. Kauli hii ya Chimera inaungwa mkono na Abawi (2013) anayebainisha kuwa lugha ya kwanza mtu hujifunza kutoka kwa wazazi wake,

Lugha ya pili ni muhimu katika jamii hizi kwani husaidia kufanikisha mawasiliano na kuleta usikilizani baina ya jamii moja na nyingine. Aidha, lugha ya pili ni kiungo cha mawasiliano katika masuala ya kibiashara, huduma za kijamii, masuala ya kidini, huduma za kiserikali na hata katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Richards (1974) anabainisha kuwa umilisi wa lugha ya kwanza ndio msingi wa kujifunza lugha ya pili. Mchakato wa kutoka lugha ya kwanza kwenda ya pili husababisha makosa kutokea kwa sababu lugha hizi mbili hutofautiana katika matamshi na katika muundo wa maneno. Mawazo haya ya Richards yanafanana na mawazo ya Kisakwah; (2014); Kische; (2016); na Nyagah; (2016). Wataalamu hawa wanasema kuwa chanzo cha makosa ya kifonolojia katika lugha ya pili ni athari za lugha ya kwanza zinazo sababishwa na wazungumzaji wa lugha ya pili.

Makala haya yamejikita katika kushughulikia makosa ya kimatamshi yanayofanywa na watu wanaoishi katika mkoa wa Mara ambao Kiswahili ni lugha yao ya pili. Imebainika kuwa watu hawa wanapokuwa wakizungumza lugha ya Kiswahili wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya makosa mbalimbali katika matamshi yao. Naye Kipacha (2016) anaeleza kuwa makosa ya kimatamshi hutokana na mabadiliko ya kifonetiki katika lugha. Suala hili husababisha kuwapo kwa kanuni zaidi ya moja kutokea katika neno linalotamkwa kimakosa. Hivyo, makosa yanayopatikana kwa

wazungumzaji wa Kiswahili katika mkoa wa Mara yamechunguzwa na kuwekwa wazi katika makala haya.

Dhana ya Matamshi

Matamshi ni dhana iliyotolewa ufafanuzi na wataalamu na watafiti mbalimbali. Darus (2005) anaeleza kuwa neno ‘matamshi’ linatokana na neno la Kiswahili *tamka* ambalo lina maana ya kutoa nje ya kinywa au pua ya mwanadamu sauti ambazo hutumika katika mazungumzo au usemaji wowote uwao. Hivyo basi, kwa kila hali neno “*matamshi*” linahusu lugha za wanadamu. Sauti hizi hutolewa kwa kufuata utaratibu maalumu. Mawazo haya hayapo mbali na mawazo ya Ndekiro (2021) anayebainisha kuwa matamshi ni utaratibu utumikao wakati wa utoaji wa sauti za maneno ya lugha ya binadamu. Kimsingi, neno *matamshi* linahusika na lugha za binadamu peke yake. Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa kuhusu matamshi, katika makala haya tunaweza kusema kuwa *matamshi* ni sauti halisi za binadamu zilizopo katika mpangilio maalumu wa kuleta maana. Sauti hizi husikika wakati wa utamkaji wa maneno ya lugha fulani baina ya mtamkaji na msikilizaji.

Mbinu za Utafiti

Data za utafiti huu zilipatikana kwa kutumia mbinu anuwai za kiutafiti. Mbinu hizo ni: mosi, kusikiliza maongezi ya watu walipokuwa nyumbani, katika shughuli za shamba, uvuvi na katika mikusanyiko ya watu vijiwani. Pili, mtafiti alihudhuria mikutano mbalimbali ya kijamii iliyomwezesha kupata data kulingana na malengo yake na tatu, data zilipatikana kutokana na masuala ya kijamii kama vile; katika taratibu za mazishi, harusi na ibada za kidini kwa lengo la kufuatilia matamshi ya lugha ya Kiswahili na kutaka kufahamu sababu za kuwapo kwa makosa ya matamshi hayo. Hivyo, chanzo kikuu cha data katika makala haya ni jamii husika. Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kwa njia ya maelezo.

Nadharia ya Utafiti

Data zilizotumika katika uandishi wa makala haya zilipatikana kwa kuongozwa na Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia iliyoasisiwa na Joan Hooper (1971). Nadharia hii ina uwezo wa kutambua chanzo cha athari za lugha na vilevile kutabiri makosa yanayotokana na athari za lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Pia, nadharia hii inasaidia kuonyesha mabadiliko ya kifonolojia na kuelezea namna ya kutumia kanuni mbalimbali katika kutatua matatizo ya kiutamkaji. Aidha, nadharia hii hudhihirisha upekee wa kila lugha. Hooper (1976), anaeleza kwamba Fonolojia Zalishi Asilia ilijikita katika kuonyesha kuwa ingawa fonolojia ilikuwa zalishi lakini uzalishi wake ulikitwa katika uasilia wa maneno yaliyokuwa yakitolewa na maumbile ya binadamu yanayohusu usemaji. Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kwamba nadharia hii ni mwafaka katika kuelezea makosa yanayojitokeza kwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili waishio katika mkoa wa Mara.

Mapitio ya Maandiko

Kipengele hiki kimeshughulikia maandiko mbalimbali yanayohusiana na suala la matamshi linaloangaziwa katika makala haya. Mochiwa (1979) alichunguza athari za Kiswahili katika lugha ya Kizigua. Katika utafiti huo alichunguza kuhusu ujuzi wa lugha, ruwaza zilizojitokeza katika matumizi ya lugha na mielekeo ya wanajamii kuhusu Kiswahili na Kizigua. Katika matokeo ya utafiti wake alibaini kuwa lugha ya Kiswahili imeiathiri lugha ya Kizigua katika matamshi na maandishi. Naye, Mbaabu (1985) anasema kuwa mtu yeyote anayejifunza lugha ngeni hufanya makosa ya kimatamshi ambayo husababishwa na ujuzi alionao katika lugha yake ya kwanza. Pia, Mgullu (1999) anaeleza kwamba makosa ya kimatamshi yanatokana na mabadiliko ya mikondo ya kifonolojia. Kila lugha inayo mikondo yake ambayo ni mahususi katika mfumo wa sauti za lugha hiyo. Anaendelea kusema kuwa fonimu fulani zinaweza kuathiriwa kwa namna fulani katika lugha moja lakini fonimu hizohizo zisiathiriane kwa namna hiyo katika lugha nyingine.

Vilevile, Kindole (2020) anafafanua kuwa makosa ya kifonolojia yanahusu sauti za matamshi halisi kuliko sauti zilizo wakilishwa katika maandishi ya kiotografia. Massamba (2006) alichunguza athari za lugha za kienyeji katika lugha ya Kiswahili mkoani Mara. Katika uchunguzi wake aligundua kuwa lugha za kienyeji zimeathiri lugha ya Kiswahili katika viwango mbalimbali vya kisarafu. Kutokana na maelezo ya watangulizi hao tunaweza kusema kuwa makosa ya kimatamshi

hujidhihirisha pale mzungumzaji wa lugha fulani anapokuwa akitoa matamshi ya lugha hiyo kwa kukokosea. Katika hali hii, dhamira na matamshi vinapishana kwa kuwa mzungumzaji humaanisha kitu kingine na katika matamshi hutamfa kitu tofauti. Naye, Ngugi (2007) alichunguza makosa ya kimatamshi kwa wanafunzi wa shule ya upili na kubaini kuwa kulikuwa na makosa ya kitahajia kwa wazungumzaji wa lugha husika yanayo dhihilishwa katika mazungumzo. Pia, Matinde (2021) anaeleza kwamba makosa ya kimatamshi hutokana na mzungumzaji kuhamisha matamshi na sauti kutoka lugha yake ya kwanza na kwenda katika lugha ya pili hilo ni tatizo linahitaji suluhu katika lugha.

Anaendelea kueleza kwamba makosa hudhihirisha dhamira ya msemaji na utamkaji halisi wa alichokusudia. Hali hii hujitokeza pale msemaji anapotamka neno visivyo tofauti na alivyodhamiria.

Kwa watu wanaoishi katika mkoa wa Mara Kiswahili ni lugha yao ya pili. Katika jitihada zao za kujifunza na kuzungumza lugha ya Kiswahili wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya makosa ya kimatamshi ambayo ni udondoshaji wa sauti, uchopekaji wa sauti uliogawanyika katika hali mbalimbali na ubadilishaji wa sauti.

Makosa ya Kimatamshi

Sehemu hii imeshughulikia makosa mbalimbali yanayofanywa na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili wa mkoa wa Mara. Makosa hayo yamejitokeza kwa namna kuu mbili, yaani udondoshaji na uchopekaji.

Makosa ya Udondoshaji wa Matamshi

Makosa ya udondoshaji wa sauti hujitokeza pale mzungumzaji anapoacha kutamka baadhi ya sauti zinazounda neno analolitamka kutokana na mfuatano wa mofimu fulani katika neno hilo. Hali hii husababisha sauti iliyokuwapo hapo awali kutoweka. Dhana hii inafafanuliwa kwa kina na Kihore, Massamba na Msanjila (2003). Wataalamu hawa wanaeleza kuwa udondoshaji ni kosa la kimatamshi ambalo husababishwa na mzungumzaji anapoacha kutamka kitamkwa fulani katika matamshi. Wanaendelea kueleza kuwa hali hii hujitokeza wakati mofimu mbili zinapokabiliana katika mazingira hayo. Kitamkwa ambacho kilikuwapo hapo awali hutoweka. Hali hii imejitokeza kwa wazungumzaji wa Kiswahili wanaoishi katika mkoa wa Mara kama ifuatavyo:

Udondoshaji wa Sauti katika Umbo la Ukanushi /h/

Wazungumzaji hawa wamekuwa na kawaida ya kudondosha sauti /h/ katika hali ya ukanushi wakati wa mazungumzo yao haliambayohusababisha uwepo wa mkosa la udondoshaji wa sauti hii katika neno. Nae, Kipacha (2016) anaeleza kuwa makosa ya kimatamshi hutokana na mabadiliko ya kifonetiki katika lugha ambayo husababisha udondoshaji, uchopekaji na ubadilishaji wa sauti, makosa haya yashughulikiwe ili lugha ibaki katika ubora wake. Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia imetuongoza katika kubaini makosa hayo, matokeo ya utafiti huu yamebainishwa hapa chini kwa kifupi. Hebu tuangalie mfano ufuatao:

1. Neno	Udondoshi
hayupo	ayupo
hukusoma	ukusoma
haji	aji

Maelezo

Udondoshaji huu wa sauti /h/ katika mfano 1 hapo juu, umejitokeza katika mazingira ya sauti /h/ kutangulia katika neno na kufuatiwa na irabu.

Kanuni

[h].....> Q /---> [+SIL]
 1 2 3 4 5 6 7

Wazungumzaji wakifuata hatua za kanuni hii wataepukana na tatizo la kudondosha sauti /h/ hata kama imetangulia katika neno la ukanushi na kufuatiwa na irabu /a/

Udondoshaji wa Sauti /u/ na /i/

Udondoshaji huu hujitokeza wakati irabu mbili zinapokuwa zimeongozana katika neno. Katika hali hii wazungumzaji hudondosha sauti moja na kuitumia sauti moja iliyosalia. Massamba na wenzake (2012) wanaeleza kuwa wazungumzaji wa lugha wanapaswa kuwa waangalifu katika kutoa matamshi sahihi ya lugha mahsusi, ili kuondoa makosa yanayojitokeza katika lugha kama vile udondoshaji, uchopekaji na ubadilishaji wa matamshi wakati wa mazungumzo. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia, mtafiti aliweza kubaini baadhi ya maneno kama ifuatavyo:

2. Neno

miimo
muumini
muungano
miili

Udondoshi

mimo
mumini
mungano
mili

Maelezo

Hivyo, sauti /u/ na /i/ itadondoshwa katika mazingira ya sauti hiyo kufuatana na sauti inayofanana nayo kama ilivyo katika mfano wa 2 hapo juu:

Kanuni

{[u] na [i]}> Q / --, --> {[u] na [i]}

1 2 3 4 5 6 7

Udondoshaji wa Sauti katika Maneno Mwambatano Yaliyoundwa na KKKI

Ontieri (2010) anabainisha kuwa wazungumzaji wa vilugha vya Kibantu mara nyingi hushindwa kutamka herufi mwambatano kwa usahihi wake. Hali hii pia imewakumba wazungumzaji wa Kiswahili katika mkoa wa Mara ambao, wanashindwa kutamka kwa usahihi baadhi ya maneno. Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ilimwongoza mtafiti kubaini makosa ya matamshi kwa wazungumzaji wa Kiswahili wanaoishi mkoani Mara. Baadhi ya makosa yaliyobainika ni kama vile:

3. Neno

kushtakiwa
kushtua

Udondoshi

kustakiwa
kustua

Maelezo

Sauti /h/ itadondoshwa katika mazingira ya sauti hiyo kutanguliwa na /s/ na kufuatiwa na /t/.

Kanuni

[h]> Q / --> [s] – [t]

1 2 3 4 5 6 7

Kanuni hii inatuonesha hatua ambazo mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili anazipitia kuidondosha sauti /h/ katika maneno hayo yenye asili ya mkopo yaliyoundwa na /K//K//K//I/. Hivyo, wazungumzaji wa Kiswahili wanaoishi mkoa wa Mara wanashindwa kutamka sauti hii na kuidondosha hali inayosababisha uwepo wa kosa la udondoshaji.

Ongezeko la Matamshi

Makosa ya kuongeza matamshi katika maneno ya Kiswahili ambayo hayahitaji ongezeko ni tatizo kubwa kwa wazungumzaji wa Kiswahili waliopo katika mkoa wa Mara. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ilibainika kuwa suala hili hujitokeza kwa kiasi kikubwa wakati mzungumzaji anapoweka msisitizo juu ya jambo fulani, anaposifia kitu fulani na anapo dunisha baadhi ya vitu. Aidha, ongezeko hujitokeza katika hali tofauti tofauti. Hebu tuangalie hali zifuatazo:

Hali ya Mazoea

Wazungumzaji wanapokuwa wakizungumzia kitu ambacho imekuwa ni mazoea yao kukitenda wamekuwa na uzoefu wa kuongeza *silabi* /ga/ katika matamshi yanayokitaja kitu hicho na *silabi* /gi/ huongezwa katika ukanushi wa kitu hicho. Sauti hizi zinzipoongezwa husababisha uwepo wa kosa la

ongezeko la kitamkwa katika neno haliinayopelekea lugha kukosa mpangilio wake mzuri wa maneno. Kwa mfano:

Neno	Uyakinishi	Ukanushi
tunakula	tunakulaga	atulagi
unacheza	unachezaga	uchezagi
anaoga	anaogaga	aogagi
wanaimba	wanaimbaga	awaimbagi

Maelezo

Hapa tunaona katika mfano hapo juu kuwa neno litaongezewa *sauti /g/* katika mazingira ya neno hilo kutumika katika hali ya mazoea ya uyakinishi.

Kanuni

Neno> ga / --> mazoea

1 2 3 4 5 6 7

Kanuni hii inaonesha kuwa mzungumzaji anaongeza sauti /g/ wakati akitamka neno ambalo imekuwa ni mazoea kutendeka. Katika ongezeko hilo anapaswa kutambua kuwa ni kosa ambalo linahalibu mpangilio wa maneno katika lugha mahsusi.

Maelezo

Katika mfano hapo juu neno litaongezewa *silabi /gi/* katika mazingira ya neno hilo kuwa katika hali ya ukanushi kwamba kitendo hicho huwa hakifanyiki. Kwa mfano:

Kanuni

Neno> gi / --> ukanushi

1 2 3 4 5 6 7

Kanuni hii inaonesha namna ambavyo mzungumzaji anavyoongeza sauti /gi/ katika neno ambalo amekusudia kufanya ukanushi, ongezeko hili ni kosa katika lugha ya Kiswahili kwani huongeza sauti ambayo haihitajiki katika neno husika.

Hali ya ukubwaishi

Wazungumzaji hawa wamekuwa wakitamka maneno kwa kuongeza *silabi /li/* katika neno ambalo mzungumzaji amekusudia kukipatia kitu hicho sifa ya ukubwa sana, unene sana, ukali sana na urefu zaidi. Ongezeko hili husababisha uwepo wa kosa la kuongeza kitamkwa katika neno ambalo halihitaji ongezeko hilo. Kwa mfano:

Neno	ukubwaishi
mguu	li - mguu
mama	li - mama
samaki	li - samaki
mti	li - mti

Maelezo

Neno litaongezwa *silabi /li/* katika mazingira ya neno hilo kuwa katika hali ya ukubwaishi.

Kanuni

Neno> li / --> ukubwaishi

1 2 3 4 5 6 7

Kanuni hii inaonesha kuwa, mzungumzaji anapokuwa akielezea kitu ambacho kipo katika hali ya ukubwa huongeza sauti /li/. Hivyo, anapaswa kutambua kuwa hilo ni kosa ambalo halipaswi kuwepo katika lugha kwani linahatarisha lugha.

Hali ya udogoishi

Wazungumzaji wa Kiswahili katika mkoa wa Mara wamekuwa na tabia ya kuongeza kitamkwa */vi/* katika maneno ambayo mzungumzaji amekusudia kukipatia sifa ya udogo zaidi au uduni sana kituambacho anakizungumzia. Hebu tuangalie mifano ifuatayo:

Neno	udogoishi
kuku	<i>vi</i> - kuku
nguo	<i>vi</i> - nguo
nyumba	<i>vi</i> - nyumba
wali	<i>vi</i> - wali

Maelezo

Neno linaongezwa kitamkwa */vi/* katika mazingira ya neno hilo kutumika katika hali ya udogoishaji.

Kanuni

Neno > *vi* / -- > udogoishi.
 1 2 3 4 5 6 7

Kama inavyoonekana katika kanuni hapo juu, wazungumzaji wanaongeza sauti */vi/* wanapokuwa wanadunisha vitu kanuni inatuelekeza hatua ambazo mzungumzaji anazipitia katika kuongeza sauti */v/* ni katika hali ya udogoishaji.

Hali ya wingi

Wazungumzaji wamekuwa na mazoea ya kuongeza kitamkwa */ma/* katika maneno ambayo hayana matamshi ya wingi ili kuyaweka katika hali ya wingi, hali hii husababisha uwepo wa kosa la kuongeza sauti katika neno ambalo halina uhitaji huo. Kwa mfano:

Neno	Ongezeko la kitamkwa
unga	<i>maunga</i>
ugali	<i>maugali</i>
nguo	<i>manguo</i>
soda	<i>masoda</i>

Maelezo

Neno litaongezwa kitamkwa */ma/* katika mazingira ya neno hili kutumika katika hali ya wingi

Kanuni

Neno > *ma* / -- > wingi
 1 2 3 4 5 6 7

Kanuni hii inaonesha kuwa wazungumzaji wanapokuwa wanazungumza neno lililopo katika hali ya wingi wamekuwa na kawaida ya kuongeza sauti */ma/* ili ni kosa la kimasamshi ambalo linaweka dosari katika mpangilio:

Ongezeko la Matamshi katika Hali ya Ukubwaishi

Ongezeko hili hufanywa na wazungumzaji wakati wanapojaribu kuelezea kitu fulani kwa kukifanya kitu hicho kuwa kikubwa sana au chakutisha sana katika maongezi yao. Kwa mfano;

Neno	Ukubwaishi
mtu	<i>limtu</i>
mama	<i>limama</i>
mti	<i>limiti</i>
samaki	<i>lisamaki</i>
chupa	<i>lichupa</i>

Maelezo

Neno litaongezwa kitamkwa */li/* katika mazingira ya neno hilo kutumika katika hali ya ukubwaishaji.

Kanuni

Neno > *li* / -- > ukubwaishi.
 1 2 3 4 5 6 7

Ongezeko la Matamshi katika Hali ya Udogoishaji

Matamshi huongezeka katika neno wakati ambapo mzungumzaji anajaribu kuvutahisia za wazungumzaji wake ili waweze kuamini kuwa kitu alichooonea ni kidogo sana. Kwa mfano;

Neno	Udogoishi
kuku	vikuku
wali	viwali
nyumba	vinyumba
nguo	vinguo

Maelezo

Neno litaongezewa kitamkwa /vi/ katika mazingira ya neno hilo kutumika katika hali ya udogoishaji

Kanuni

Neno	> vi / --		> udogoishi.
1	2	3 4 5	6 7

Makosa ya Ubadilishaji wa Sauti

Baadhi ya wazungumzaji wa Kiswahili wanaoishi katika mkoa wa Mara wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya kubadilisha baadhi ya sauti wanapokuwa katika mazungumzo yao. Hali hii inajitokeza wakati wazungumzaji hao wanapokuwa wameshindwa kutofautisha sauti ambazo zinakuwa na baadhi ya sifa zinazofanana katika matamshi. Mbaabu (1985) anaelezea kuwa matatizo ya kimatamshi yanayojitokeza katika lugha ya pili husababishwa na umilisi wa matamshi wa lugha ya kwanza alionao mzungumzaji ambao husababisha makosa ya kifonolojia katika lugha ya pili. Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ilisaidia kubaini baadhi ya wazungumzaji ambao wanakabiliwa na makosa ya ubadilishaji wa sauti kama ifuatavyo:

Ubadilishaji wa Sauti /l/ na Kutamka Sauti /r/

Kitamkwa /l/ hubadilishwa wakati wa utamkaji na badala yake huwekwa kitamkwa /r/. Tatizo hili hujitokeza pale mzungumzaji anaposhindwa kutofautisha utamkaji wa sauti hizi kwa kuwa zote ni sauti za ufizi. Mtamkaji anashindwa kuzitofautisha sauti hizi wakati wa utamkaji kwani /r/ ni kimadende na /l/ ni kitambaza. Kutokana na kushindwa kupata tofauti hizi makosa ya ubadilishaji hutokea. Mfano ufuatao unadhihirisha suala hilo.

Neno	Badiliko
amelala	amerara
amekula	amekura

Maelezo

Sauti /r/ hubadilishwa na kuwa sauti /l/ katika mazingira ya sauti hizi kutamkiwa katika eneo moja la ufizi.

Kanuni

r	> l / --		> ufizi
1	2	3 4 5 6	7

Ubadilishaji wa Sauti /ga/ badala ya /gh/

Kutamka *silabi* /ga/ badala ya /gh/. Sauti hizi zinawachanganya wazungumzaji kwa sababu zote ni sauti zinazotamkiwa katika kaakaa laini.

Sababu za Kuwapo kwa Makosa ya Kimatamshi

Hooper (1976) anaelezea Nadharia ya Fonolojia Zalishi kwamba ina uwezo wa kuonesha umilisi wa wazawa wa lugha unaomuwezesha kutoa matamshi yasiyo na kikomo. Hivyo, nadharia hii imetumika kutuongoza katika kupata sababu za kuwapo kwa makosa ya kimatamshi. Wakazi wa mkoa wa Mara wana lugha *zao* za kwanza na Kiswahili ni lugha yao ya pili. Watu hawa wamekuwa na lugha *zao* za kwanza ambazo zimekuwa zikiwasaidia katika mawasiliano mbalimbali. Baada ya kuona kuwapo kwa hitaji la kutumia lugha ya Kiswahili waliamua kujifunza kuongea lugha hiyo.

Richards (1971) anabainisha kwamba umilisi wa lugha ya kwanza ndio msingi wa kujifunza lugha ya pili. Hii ina maana kwamba uzoefu wa lugha ya kwanza huhamishwa kwenda lugha ya pili ambayo mtu anataka kujifunza. Richards anaendelea kueleza kuwa katika harakati za uhamishaji makosa mengi hutokea kwasababu lugha hizi hutofautiana katika matamshi na katika muundo wa maneno. Uhamishaji huo wa ujuzi wa lugha ya kwanza katika Kiswahili ndio uliosababisha makosa kutokea kwa wazungumzaji wa Kiswahili waishio katika mkoa wa Mara.

Mazingira ya Ujifunzaji wa Lugha ya Pili

Ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa wakazi wa mkoa wa Mara unakuwa mgumu kwasababu watu hujifunza lugha wakiwa katika mazingira yao ambamo wamekuwa wakizungumza lugha zao za kwanza. Kwa hali hii, milango yao ya fahamu imezoea uwepo wa lugha yao, hivyo, hushindwa kutofautisha lugha ngeni na lugha iliyozoeleka. Hali hii husababisha makosa kujitokeza wakati wa kujifunza lugha ya pili. Makosa hayo ni pamoja na kubadilisha sauti, kudondosha sauti fulani na hata kuchopeka sauti fulanifulani katika lugha wanayojifunza kutokana na kujifunzia lugha yao ya pili katika mazingira yaleyale waliyoyazoea katika matumizi ya lugha zao za kwanza. Gas (1979) anasema kuwa lugha inayofunzwa katika jamii ambamo kuna lugha inayotumika zaidi katika mawasiliano ya kila siku, inaweza kuathiriwa kwa sababu ya kuwapo kwa matumizi ya lugha nyingine katika mazingira ya jamii husika. Watu wa mkoa wa Mara wamejifunza lugha ya Kiswahili katika mazingira ambamo lugha zao za kwanza hutumika. Hali hii imesababisha kuwapo kwa makosa ya udondoshaji wa sauti, ubadilishaji wa sauti na uongezaji wa sauti katika baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili.

Uhaba wa Walimu Mahiri

Utafiti huu umebaini kuwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili waishio mkoa wa Mara katika harakati zao za kujifunza Kiswahili wanakabiliwa na uhaba wa walimu wenye sifa stahiki za kufundisha lugha ya pili. Imebainika kuwa wakazi hao wa mkoa wa Mara wamekuwa wakitumia juhudi zao binafsi katika kujifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili. Mtafiti amebaini kuwa watu hao wamekuwa wakijifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili kwa njia ya kusikiliza na kuiga kile kilichoongelewa na mtu mwingine. Ikitokea yule anayesikilizwa na kuigwa hana umilisi wa kutosha watu huiga na kujifunza makosa. Abawi (2013) anasema kuwa, mwanafunzi anapaswa kufundishwa vitu rahisi kwenda vitu vigumu. Kitu cha kwanza katika ufundishaji ni salamu ili anayefundishwa aweze kupata mawasiliano ya awali. Utaalamu huu wa kuwakusanya watu vijijini na kuwaweka pamoja kwa lengo la kuwafundisha lugha katika mkoa wa Mara haupo. Hali hiyo inasababisha watu kujifunza mitaani kwa juhudi zao binafsi na kuongea wanavyoweza kwa kadri walivyojifunza. Wasomi wachache waliobahatika kufundishwa darasani ndio walio na uelewa wa kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha. Naye, Msigwa (2020) anasema kuwa watu wazima wanaojifunza lugha ya pili hujifunza kwa hiari yao wenyewe wakiwa na malengo yao, hivyo hujitahidi kutumia milango yao ya fahamu kwa kuhusianisha vitu halisi walivyonyavyo katika lugha yao ya kwanza na kuvihamishia katika lugha wanayojifunza. Huu ni mchakato wa kiutambuzi unaofanywa na watu wazima kwa sababu ya ukosefu wa walimu.

Upungufu wa Zana za Kufundishia na Kujifunzia Shuleni

Hili ni tatizo kwa walimu na wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili katika mfumo rasmi (shuleni) Kutokana na kukosekana kwa zana wanafunzi hawapati maarifa kwa usahihi na ukamilifu kwani kuna baadhi ya vitu ambavyo ni ngumu mwalimu kuelezea akaeleweka vizuri bila zana hizo Inabidi mwanafunzi aone, aguse, aonje ndipo aweze kuelewa vizuri. Kutokana na hali hii makosa ya kimatamshi katika lugha hujitokeza.

Hitimisho

Makala haya yamechunguza makosa ya kimatamshi katika mkoa wa Mara. Makala imebaini kwamba yapo makosa ya kimatamshi yanayofanywa na wakazi wa mkoa wa Mara nayo ni ubadilishaji wa sauti, udondoshaji wa sauti na ongezeko la sauti ambalo limegawanyika katika sehemu mbalimbali kulingana na muktadha wa mazungumzo. Pia makala imebaini kanuni zilizosababisha makosa hayo kutokea. Aidha, makala imeweka wazi mambo yanayosababisha kuwapo kwa makosa hayo ambayo ni: uhaba wa walimu mahiri, upungufu wa vifaa, uzoefu wa lugha ya kwanza na mazingira ya

ujifunzaji. Hivyo sababu hizi ndizo zinazofanya wanaojifunza lugha ya Kiswahili kushindwa kumudu kuzungumza Kiswahili fasaha. Suala la uhawilishaji linapaswa kufanyika kwa kuzingatia sababu zilizobainika katika makala haya ili kuwapatia wajifunzaji mazingira rafiki ya kujifunza.

Marejeleo

- Abawi, L. (2013). School Meaning Systems: The Symbiotic Nature of Culture and 'Language-in-Use.' *Improving Schools*, 16(2), 89–106. Retrieved from <http://journals.sagepub.com/doi/10.1177/1365480213492407>
- Chimerah, R. (1998). *Kiswahili Past Present and Future Horizons*. Nairobi University Press.
- Chomsky, N., & Morris, H. (1968). *The Sound Pattern of English* (ERIC Ed.). Institute of Education Sciences FAQ.
- Dane, F. C. (1990). *Research Methods*. Thomason Books Publishing Co.
- Darus. (2005). *Athari za Lugha katika Lugha ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Gas, S. (1979). Language Transfer and Universal Grammatical Relations. *Language Learning*, 29(2), 327–344. Retrieved from <https://onlinelibrary.wiley.com/doi/10.1111/j.1467-1770.1979.tb01073.x>
- Khansir, A. A. (2012). Error Analysis and Second Language Acquisition. *Theory and Practice in Language Studies*, 2(5), 1027–1032.
- Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B., & Msanjila, Y. P. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*. Chuo kuu cha Dar es Salaam.
- Kindole, E. (2020). Matumizi ya Alama za Kifonetiki za Kimataifa katika Uwasilishaji wa Taarifa za Kimatamshi katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la 3. *Kioo cha Lugha: Journal of Language, Technology & Entrepreneurship in Africa*, 17(1).
- Kipacha, A. (2016). *Utangulizi wa Lugha na Isimu OSW 101*, (August).
- Kisakwah, B. A. (2014). *Uchanganuzi Makosa na Muundo Sentensi: Ulinganisho wa Sentensi Sabili za Kiswahili Sanifu na za Kisuba*. University of Nairobi.
- Kishe, A. (2016). Kuingiliana kwa Lugha ya Kiswahili na Kiingereza: Uwasilishaji wa Maneno ya Kiingereza. *Huria: Journal of the Open University of Tanzania*, 21(1), 91–105.
- Massamba, D. P. B. (2006). *Kiswahili cha Musoma: Mwanzo wa lahaja Nyingine. Kiswahili*. Serengeti Publisher.
- Matinde, R. S. (2021). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia: Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na vyuo Vikuu*. Serengeti Educational Publishers Limited.
- Mbaabu, I. (1985). *New Horizons in Kiswahili: A Synthesis in Developments, Research, and Literature*. Kenya Literature Bureau.
- Mgullu, R. S. (1999). *Mtala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Longhorn Publishers.
- Mochiwa, Z. S. M. (1979). *The Impact of Kiswahili Language on Ethnic Languages: A Case Study from Handeni District*. University of Dar es Salaam.
- Msigwa, A. B. G. (2020). *Kioo cha Lugha*, 18, 22–35.
- Ndekiro, R. (2021). Sababu za Matumizi ya Lugha Tandawazi katika Mtandao wa Facebook na Athari zake katika Kiswahili Sanifu. *Mulika Journal*, 39(16).
- Ngugi, J. K. (2007). *Uchunguzi wa Athari za Kifonolojia Miongoni mwa Wanafunzi Wakikanyu: Mfano kutoka katika Tarafa ya Babati, Nakuru*. Chuo Kuu cha Egerton.
- Nyagah, S. K. (2016). *Uchanganuzi wa Makosa ya Kifonolojia na Kimofolojia Yanayojitokeza katika Kazi Andishi za Wanafunzi wa Shule za Upili Tigani Jimboni Meru*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Nairobi: Chuo Kuu cha Nairobi.
- Ontieri, J. O. (2010). *Uchunguzi wa Makosa katika Insha za Wanafunzi wa Shule za Upili. Mfano wa Wilaya ya Nakuru*. Chuo Kuu cha Egerton. Tigania Jimbo la Meru. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Nairobi: Chuo Kuu cha Nairobi.
- Richards, J. (1974). Analysis, Perspective on Second Language Acquisition in J. C. A. Mon Contractive Aproach to Error Analysis. *Africa Education Review*, 2, 172–188.
- Richards, J. (1971). *Error Analysis and Second Language Strategies*. Language Sciences.